CAPITAL MARKETS AND SECURITIES AUTHORITY

MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA

MWONGOZO KWA WAWEKEZAJI KATIKA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA TANZANIA

MWONGOZO KWA WAWEKEZAJI KATIKA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA.

1. Masoko ya Fedha

Masoko ya fedha ni masoko yenye kuhusisha dhamana zinazomilikiwa na wadau mbalimbali. Masoko haya yamegawanyika katika sehemu kuu mbili: masoko ya mitaji na masoko ya fedha. Masoko ya mitaji ni masoko yanayohusisha dhamana za muda mrefu. Haya ni masoko ya dhamana na mitaji yenye kuiva baada ya muda wa zaidi ya mwaka mmoja. Masoko ya fedha yanahusika na dhamana za muda mfupi ambazo ni pungufu ya mwaka mmoja.

Madhumuni makubwa ya masoko ya mitaji ni kusaidia ukusanyaji wa mitaji kutoka kwa umma wa wawekezaji na pia kuwezesha uhamishaji wa rasilimali kutoka kwa wenye mitaji kwenda kwa wenye kuhitaji mitaji hiyo kupitia masoko ya mitaji. Masoko haya yanadhaniwa kuwa nafuu na yenye ufanisi wa hali ya juu. Wahusika wakuu wanaweza kuwa ni wananchi wa kawaida, kampuni za kibiashara, serikali kuu pamoja na serikali za mitaa. Kwa ujumla, serikali kuu, serikali za mitaa na kampuni za biashara wanahitaji mitaji kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku kama vile ujenzi wa barabara, mabwawa, viwanda n.k. Wananchi na baadhi ya taasisi nyingine ni wenye mitaji inayohitaji sehemu za kuwekeza.

Lengo ni kuhamisha mitaji kutoka kwa wenye kuimiliki kwenda kwa wahitaji ambao watawekeza kwenye rasilimali zinazozalisha. Hii huweza kufanyika moja kwa moja au kupitia njia mbadala. Bila kujali njia ya kuhamisha mitaji husika, kinachotegemewa ni kukutana kwa wahusika wakuu kwenye ubadilishanaji huo kwa gharama nafuu na bila ya usumbufu mkubwa.

2. Dhana ya Thamani ya Fedha

Bei ya hisa na dhamana katika soko la mitaji hubadilika kwa kupanda au kushuka kutokana na hali ya soko na uchumi kwa ujumla, hivyo kumweka mwekezaji kwenye mazingira ambayo yanamfanya aweze wakati mwingine kupata faida ama hasara. Mfano mtu anaponunua hisa anakuwa amewekeza. Ile fedha ambayo angeitumia kwa matumizi ya kawaida inawekwa kwenye hisa na hivyo haipo kwa matumizi hayo. Akitaka kuitumia baadaye atauza hisa zake na kupata fedha hiyo. Kuna uwezekano kuwa wakati anataka kuitumia, fedha hiyo haitamwezesha kununua idadi ya mahitaji yake kama ambavyo angeitumia leo.

Hii inatokana na kupungua kwa thamani ya fedha sababu ya mfumuko wa bei. Mwekezaji anahitaji kufidiwa kutokana na mfumuko wa bei. Dhana hii ndio inaitwa dhana ya thamani ya fedha. Kwa maneno mengine, thamani ya fedha ya leo sio sawa na kesho kutokana na mfumuko wa bei. Thamani hii inakuwa tofauti kwa sababu ya mfumuko wa bei. Iwapo mwekezaji atahitaji kutumia idadi ya bidhaa zilezile ambazo angetumia kwa sasa, anahitaji namna ya kufidia upungufu huo. Riba ni njia mojawapo ya kufidia upungufu huo.

Uwekezaji unalenga kumfidia mwekezaji kutokana na faida inayopatikana ambayo inatakiwa kuziba pengo hilo. Kwa mfano kama mwekezaji anahitaji sukari kilo 100 kwa mwaka, na akaamua kutonunua sukari mwaka huu na kuweka fedha yake kwenye hisa, inategemewa kuwa faida atakayopata itamwezesha kununua kilo 100 za sukari mwaka mmoja tokea sasa. Ili aweze kupata kilo 100, ni lazima uwekezaji wake umpatie faida ya kufidia kupanda kwa bei ya sukari ifikapo muda wa kuhitaji bidhaa hiyo. Faida ya uwekezaji ndio fidia yenyewe ya kumwezesha kununua kilo 100 za sukari mwaka unaofuata.

Wawekezaji wana njia mbalimbali za kuwekeza. Kwa kutumia mbinu tofauti, wawekezaji huweza kuwekeza na kupata faida inayotegemewa kuwafidia pale thamani ya fedha inaposhuka. Sehemu hizi za uwekezaji zimegawanyika kwenye mafungu mawili ambayo ni:

2.1. Dhamana za masoko ya fedha

Dhamana hizi ni pamoja na hawala za serikali, amana za benki, amana za muda maalum za kampuni. Dhamana hizi ni za muda mfupi, yaani zinazoiva ndani ya mwaka mmoja au pungufu yake)

2.2. Dhamana za masoko ya mitaji

Kwenye masoko ya mitaji, dhamana hizi ni pamoja na hisa, hatifungani na

vipande vya mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Dhamana hizi zinaiva baada ya mwaka mmoja au zaidi)

3. Uwezekano wa kupata hasara dhidi ya faida

Uwezekano wa kupata hasara ni uwezekano wa mapato ya baadaye kuwa tofauti na mapato yanayotarajiwa na mwekezaji. Hii inatokana na uwezekano wa mambo kadha wa kadha kutokea. Mwekezaji anavyowekeza fedha zake kwenye masoko ya mitaji na dhamana, anakuwa tayari amekubali uwezekano wa kupata hasara ama faida. Hii ni pamoja na uwezekano wa kutorudishiwa fedha zilizokopwa (kwa wawekezaji wa hatifungani); ufanisi mdogo wa kampuni ambapo mwekezaji amewekeza fedha zake, hii inaweza kusababisha bei ya hisa husika kuanguka; mabadiliko ya riba kwenye uchumi wa nchi yanayoweza kuathiri mauzo na manunuzi ya hisa kwenye soko la hisa; pamoja na mabadiliko mengine ambayo yatakuwa na athari kwenye thamani ya hisa na dhamana zilizoko kwenye masoko ya mitaji kwa mfano mfumuko wa bei, mabadiliko ya kodi na mabadiliko ya sheria za nchi.

Kila uwekezaji una faida na hatari zake na pia hatari hizi zinatofautiana. Tofauti za hatari husababisha tofauti ya faida itolewayo na uwekezaji husika. Kwa kawaida, uwekezaji wenye hatari kubwa unatakiwa kuwa na faida kubwa ili kumfidia mwekezaji kiwango cha hatari anachokichukua kwenye uwekezaji wake.

Utayari wa mwekezaji kuwekeza kwenye maeneo yenye hatari, ndio utamsaidia kuchagua awekeze kwenye kitega uchumi kinachoendana na utayari wake wa kupoteza mtaji wake. Kwa maneno mengine, mwekezaji aliye tayari kupata faida kubwa vivyo hivyo uwezekano wa kupata hasara unakua mkubwa hali inayoweza

kusababisha kukosa uhakika mkubwa wa kurudishiwa mtaji wake. Mwekezaji huyu atachagua kitega uchumi kilicho na uwezo unaolingana na utayari wake kupoteza mtaji, na hivyo kuhitaji faida inayoendana na hatari aliyoibeba.

Kwa hiyo ili kuamua kuwekeza kwenye chombo fulani cha uwekezaji, kuna haja ya kutofautisha uwezekano wa kupata hasara katika uwekezaji ili kufikia uamuzi ni kiasi gani kinawekezwa kwenye kitega uchumi kimoja hadi kingine, na kama mwekezaji atawekeza kwenye masoko ya mitaji au masoko ya fedha.

Pia hatari za uwekezaji zinasaidia kufikia uamuzi wa kuwekeza kwa muda mfupi au muda mrefu.

4. Dhamana za masoko ya fedha

Hizi ni dhamana za uwekezaji zisizozidi mwaka mmoja. Dhamana hizi huiva ndani ya siku 364 au pungufu ya hapo. Uwekezaji huu unajumuisha vitega uchumi vya muda usiozidi mwaka mmoja tangu mwekezaji aweke fedha yake kwenye vyombo hivi. Wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwa muda mfupi hutumia vyombo hivi ili kukidhi mahitaji yao ya fedha na pia kwa kuwa wanaogopa kupoteza mitaji yao. Wawekezaji hawa hupenda kurudisha uwekezaji wao chini ya mwaka mmoja kwa kutumia vyombo vya uwekezaji vifuatavyo:

4.1. Dhamana za serikali kuu

Hivi ni vyombo vya uwekezaji wa muda mfupi kati ya siku 35 hadi siku 364 vinavyotolewa na serikali kuu kupitia benki kuu ya Tanzania. Dhamana za serikali hutumika kama njia ya kuboresha uchumi kwa kupanga mzunguko wa fedha kwenye uchumi wa nchi ili kudhibiti mfumuko wa bei na riba za mabenki. Mnada wa dhamana za serikali hufanyika kila wiki siku ya Jumatano. Wawekezaji wanaruhusiwa kupeleka maombi yao ya kuwekeza moja kwa moja benki kuu kwa wawekezaji wenye fedha zaidi ya shilingi za kitanzania milioni tano. Wawekezaji wengine ambao hawana kiasi hicho cha fedha wanaweza kuwekeza kupitia mawakala maalum wa benki kuu ambao ni pamoja na mawakala wa soko la hisa na mabenki.

4.2. Amana za benki

Hizi ni amana za muda maalum zinazotolewa na mabenki mbalimbali.

4.3. Uwekezaji wa muda kwenye kampuni

Hizi ni amana za muda maalum zinazotolewa na kampuni ili kupata mitaji ya kufanyia shughuli zao.

5. Dhamana za masoko ya mitaji

Masoko ya mitaji ni masoko ya fedha yenye kuhusisha dhamana za uwekezaji za muda mrefu zaidi ya mwaka mmoja. Vyombo hivi ni vya muda mrefu na mtoaji hahitaji kurudishia wawekezaji fedha zao, bali wawekezaji wanaweza kupata fedha zao kwa kuuza dhamana hizi kwenye masoko ya mitaji. Kwa kawaida, dhamana

hizi huuzwa kwenye masoko ya hisa ili kusaidia wawekezaji kuweza kutoka na kuingia kwenye uwekezaji na pia kufahamu thamani ya uwekezaji wao. Kwa kawaida, wawekezaji wenye kushiriki kwenye masoko ya mitaji wana mpango wa ushiriki wa muda mrefu na urahisi wa kujitoa kutoka uwekezaji sio lengo kuu. Lengo kuu la mwekezaji wa muda mrefu ni faida kubwa. Wawekezaji wa muda mrefu wako tayari kuwekeza kwenye vitega uchumi vyenye uwezekano mkubwa wa hasara na faida kuliko wale wa muda mfupi kwa sababu wanategemea kupata faida kubwa.

Miongoni mwa dhamana maarufu au zinazojulikana na wengi kwa upande wa uwekezaji kwenye masoko ya mitaji ni pamoja na hisa (ambazo ni sehemu ya umiliki wa kampuni), hatifungani - ambalo ni deni lililotolewa na mwekezaji kwa kampuni, serikali kuu au za mitaa na ambalo litalipwa baada ya muda wa deni hilo kuisha. Deni hilo lina muda maalum wa kulipwa na mkopaji analipa riba iliyokubaliwa. Chombo kingine cha uwekezaji wa muda mrefu ni vipande vya mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Vipande vinawakilisha sehemu ya umiliki wa uwekezaji wa pamoja ambao umewekeza fedha iliyokusanywa kwenye vitega uchumi mbalimbali kama vile hisa, hatifungani, dhamana za serikali kuu, amana za muda maalum n.k.

Uwekezaji kwenye hisa una uwezekano mkubwa zaidi wa hasara kulinganisha na uwekezaji kwenye vyombo vingine vya uwekezaji wa muda mrefu. Hii inatokana na ukweli kwamba riba ya hatifungani hulipwa kabla ya faida ya uwekezaji kwenye hisa. Hivyo mwekezaji kwenye hatifungani ana uhakika mkubwa wa malipo kuliko mwekezaji kwenye hisa. Pia iwapo kampuni itafilisika, mwekezaji kwenye hatifungani atalipwa madai yake kabla ya wenye hisa kulipwa kutokana na mauzo ya rasilimali za kampuni. Kwa upande mwingine, hatifungani za serikali kuu zinaaminiwa kuwa hazina uwezekano wa hasara (risk free) kwa sababu serikali ina uwezo wa kutoza kodi, na kuchapisha fedha, hivyo wawekezaji wana uhakika mkubwa wa kulipwa riba na mitaji yao kuliko wawekezaji kwenye hisa na vipande. Uwezekano wa hasara unaozungumziwa ni kushindwa kulipwa na wakopaji na kampuni. Hata hivyo kuwepo kwa hatari ya kushindwa kulipa hakuondoi hatari nyingine kama vile mabadiliko ya riba na hali halisi ya masoko ya mitaji.

5.1. Vyombo vya uwekezaji kwenye madeni

5.1.1. **Tofauti itokanayo na mtoaji:**

Hatifungani zinaweza kutolewa na taasisi mbalimbali kama vile kampuni, serikali kuu na serikali za mitaa. Hatifungani zitolewazo na kampuni huitwa hatifungani za kampuni. Zile zitolewazo na serikali kuu huitwa hatifungani za serikali kuu, na zinazotolewa na serikali za mitaa huitwa hatifungani za serikali za mitaa. Hadi kufikia Agosti 2010, soko la hisa la DSM lina hatifungani za serikali kuu na kampuni tu. Hatifungani za serikali kuu zipo takribani 168 na hatifungani za makampuni binafsi zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam zisizopungua 6.

5.1.2. **Tofauti itokanayo na namna ya kulipa riba:**

Mtoaji wa hatifungani anaweza kulipa riba isiyobadilika kwa kipindi chote cha kuwepo hatifungani hiyo au riba inayobadilika kutokana na kubadilika kwa kigezo cha kupanga riba iweje. Riba isiyobadilika huwa inalipwa muda wote wa kuwepo kwa hatifungani hiyo. Hatifungani inayolipa riba inayobadilika hutumia kitega uchumi kingine kupanga riba itakayolipwa, mfano dhamana za serikali kuu za siku 182 hutumika kama kigezo cha kupanga riba itakayolipwa na benki ya maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB) kwa wawekezaji kwenye hatifungani ya benki hiyo. Benki hii imeongeza asilimia 0.75% juu ya riba ya siku 182 kupanga riba itakayolipwa kwenye hatifungani yake. Kigezo hiki huangaliwa kila baada ya miezi sita, na riba ikishapangwa hutumika kutafuta jumuisho la riba hadi itakapolipwa tena baada ya miezi sita. EADB II inalipa riba kila Julai na Januari ya kila mwaka.

Hatifungani zisizolipa riba ni hatifungani ziuzwazo na watoaji wa hatifungani hizi ambapo wawekezaji hulipa fedha pungufu ya thamani ya hatifungani na kuahidiwa kulipwa thamani kamili ya hatifungani. Mfano, mtoaji anaweza kutoa hatifungani kwa kuiuza kwa TZS 98 kwa ahadi kuwa atarudisha TZS 100 kwa kila hatifungani muda wa malipo utakapofika. Kwa kipindi chote cha kuwepo kwa hatifungani hiyo, mwekezaji hatalipwa riba. Faida apatayo mwekezaji ni wakati wa kuirudisha kwa mtoaji ambapo atalipwa TZS 100. Faida ni tofauti ya bei aliyolipa wakati wa kuwekeza na bei atakayopokea wakati wa kurudishiwa mtaji wake.

5.2. Hisa

Masoko ya hisa huuza na kununua hisa za kampuni yaliyoorodheshwa kwenye masoko ya mitaji. Hisa husika zinaweza kuwa ni hisa za kawaida na hisa za upendeleo. Kwa sasa (Disemba 2019) soko la hisa lina jumla ya hisa za kawaida za kampuni 27 ambazo zimeorodheshwa ikiwa ni pamoja na hisa za kawaida za kampuni 6 kutoka Kenya. Hakuna hisa za upendeleo kwenye soko la hisa la DSM kwa sasa.

5.3. Tofauti za hisa mbalimbali

Hisa zinatofautiana kutokana na vigezo mbalimbali. Hisa za kawaida humwezesha mwekezaji kurudishiwa mtaji wake akiwa mdau wa mwisho baada ya wadau wengine wote kulipwa kutokana na mauzo ya rasilimali za kampuni. Hii hutokea kampuni inapofilisiwa. Pia kiwango cha gawio kinacholipwa hakijulikani tangu awali. Hisa za upendeleo zina kiwango maalumu cha gawio ambacho hulipwa kutokana na faida ya kampuni. Wenye hisa za kawaida hubeba uwezekano mkubwa wa hasara kuliko wenye hisa za upendeleo kutokana na tofauti iliyoelezwa hapo juu.

5.3.1. **Tofauti kati ya hisa za kawaida na za upendeleo:**

Hisa za kawaida zinawakilisha sehemu ya umiliki wa kampuni. Kama kampuni ina hisa milioni moja na mwekezaji ana hisa 10,000, basi

mwekezaji huyo atakuwa anamiliki 1% ya kampuni hiyo. Kama kampuni itaamua kulipa gawio kutokana na faida iliyopatikana, basi mwekezaji huyo atapokea 1% ya gawio. Na iwapo kampuni itapata hasara, mwekezaji huyo atabeba 1% ya hasara iliyopatikana.

Hisa za upendeleo kwa upande mwingine ni sehemu ya umiliki ikiwa na maslahi tofauti na hisa za kawaida. Hisa za upendeleo ni namna yakampuni kupata mtaji kupitia vyombo vya uwekezaji vinavyofanana na hisa za kawaida na pia vyenye kufanana na hatifungani. Hisa hizi zinafanana na hisa za kawaida kwa sababu zina madai dhidi ya mali za kampuni. Aidha, zinafanana na hatifungani kwa sababu zinalipwa gawio kabla ya hisa za kawaida, zinalipwa gawio lenye kufahamika.

Kushindwa kulipa gawio la hisa za upendeleo hakusababishi kampuni kufilisiwa kama ilivyo kwenye hatifungani na madeni mengine kama ya benki. Gawio la hisa za upendeleo linaweza kuwa linalundikana (cumulative) hadi hapo kampuni itakapokuwa na uwezo wa kulipa gawio. Gawio la nyuma ni lazima lilipwe kabla ya hisa za kawaida kulipwa gawio.

5.4. Faida za kuwekeza kwenye hisa

Kuwekeza kwenye hisa kuna faida zifuatazo:

- Ni njia ya kuweka akiba - kununua hisa ni kuwekeza kwa matumizi ya baadaye;
- Kuna nafuu ya kodi ya zuio kwenye gawio ya 5% kwa makampuni yaliyoorodheshwa kwenye soko la hisa kulingana na 10% kwa yale yasiyoorodheshwa;
- Hakuna kodi ya ongezeko la thamani kwa kampuni yaliyo kwenye soko la hisa ikilinganishwa na 10% kwa yale yasio kwenye soko la hisa;
- Kunawezesha umiliki wa makampuni;
- Kunawezesha kushiriki kwenye mgao wa hisa za bakshishi;
- Kunampa mwekezaji fursa ya kutoa maoni yake kwenye mkutano mkuu wa kampuni;
- Hisa zinaweza kuwekwa rehani kupata mkopo.

Faida za kuwekeza kwenye hatifungani

Riba ni faida itokanayo na uwekezaji kwenye hatifungani. Uwekezaji kwenye hatifungani una hatari ya uwekezaji kidogo kuliko uwekezaji kwenye hisa. Kiwango cha riba kinajulikana tofauti na gawio ambalo hutegemea faida ya kampuni. Wawekezaji kwenye hatifungani wanapewa kipaumbele wakati wa malipo. Kutokana na hayo, mapato ya uwekezaji kwenye hatifungani kwa kawaida yanakuwa madogo kuliko gawio kutokana na uhakika huo. Pia riba hulipwa bila kuangalia ufanisi wa kampuni, na ni sehemu ya gharama za uendeshaji wa kampuni.

5.6. Faida za kuwekeza kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja

Uwekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja ni njia mbadala ya kuwekeza kwenye masoko ya mitaji. Mifuko hii humwezesha mwekezaji kutawanya uwekezaji wake sehemu mbalimbali kulingana na sera ya mfuko. Mifuko hii pia husimamiwa na wataalamu wenye uzoefu wa uwekezaji na hivyo kusaidia kupunguza uwezekano wa kupata hasara katika uwekezaji. Mifuko ya uwekezaji wa pamoja pia ina faida ya kuwezesha wawekezaji wenye akiba kidogo kuwekeza kwani bei ya vipande ni ndogo inayoweza kulipiwa na wenye vipato vya chini na wasioweza kushiriki kwenye masoko ya mitaji moja kwa moja.

Gharama za mifuko hii hubebwa na mifuko yenyewe.

Hadi Desemba, kulikuwa na mipango 8 ya uwekezaji wa pamoja ambayo ni Mfuko wa Umoja, Wekeza Maisha, Jikimu, Mfuko wa Watoto, Ukwasi, Mfuko wa hati Fungani na kampuni za NICO na TCCIA Investment Limited. NICO na TCCIA ni mifuko ya uwekezaji wa pamoja kwa mfumo wa kampuni ya uwekezaji.

6. Kwa nini bei ya hisa hubadilika?

Hisa ni kama bidhaa nyingine yeyote ambayo thamani yake hufahamika kutokana na nguvu ya soko. Mauzo na manunuzi ya hisa kwenye soko la hisa hetegemea mambo mengi ikiwa ni pamoja na:

6.1. Ufanisi wa kampuni

Kampuni zinazopata faida huwavutia wawekezaji kuwekeza kwenye kampuni hizo. Kwa vile idadi ya hisa haibadiliki, inapotokea wawekezaji wanataka kuwekeza kwenye kampuni kutokana na ufanisi wake, basi hutokea bei ya hisa hizo kuongezeka. Kama kampuni haitakuwa na ufanisi mzuri, bei ya hisa zake pia hupungua.

6.2. Hali ya uchumi wa nchi kwa ujumla

Uchumi wa nchi huwezesha wananchi kuwa na mapato ambayo huwekezwa kwenye masoko ya fedha. Mwenendo mzima wa uchumi wa nchi husababisha ufanisi wa makampuni kubadilika kutokana na mwelekeo wa uchumi husika, na hivyo kusababisha kubadilika kwa bei za hisa kwenye masoko ya mitaji.

6.3. Sera za serikali

Hizi ni sera zinazotolewa na serikali kuhusu masuala mbalimbali. Iwapo sera ina athari mbaya kwa kampuni, basi ufanisi wa kampuni husika utaathirika na kusababisha kupungua kwa bei ya hisa kwenye soko la hisa. Iwapo sera inafaidisha makampuni,basi bei ya hisa zake itaongezeka.

6.4. Taarifa yoyote yenye kuathiri bei ya hisa

Kuna matukio mbalimbali ambayo yanaweza kuwa na athari kwenye bei ya hisa. Hii ni pamoja na mabadiliko ya viongozi wa taasisi, kupatikana kwa masoko

mapya, kuuzwa kwa sehemu ya kampuni n.k Haya yote yataathiri ufanisi wa kampuni na bei ya hisa zake sokoni.

7. Vigezo muhimu kwenye uwekezaji

Ili kufanya maamuzi kuhusu uwekezaji, mwekezaji anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

Mategemeo ya faida na uwezekano wa kupata hasara katika uwekezaji – faida ya uwekezaji ndio lengo kuu la kuwekeza kwenye masoko ya mitaji mahali popote duniani. Faida za uwekezaji hutokana na gawio, riba na au ongezeko la thamani ya uwekezaji. Faida hii inaweza kuongezeka au kupungua kulingana na mategemeo ya mwekezaji. Mabadiliko haya ndiyo yanafahamika kama uwezekano wa kupata hasara katika uwekezaji. Mwekezaji anayetaka faida kubwa anatakiwa kukubali uwezekano mkubwa wa hasara katika uwekezaji.

Urahisi wa kuuza hisa/dhamana – masoko ya mitaji yanategemewa kumsaidia mwekezaji kuuza rasilimali yake na kupata fedha taslimu. Dhamana zenye soko kubwa zinapendwa na wawekezaji zaidi kuliko zisizo na soko. Uamuzi wa kuwekeza utazingatia urahisi wa kuuza pia.

Kuwepo kwa uwekezaji mbadala na faida zake – uwekezaji mbadala unatoa fursa kwa mwekezaji kuamua awekeze wapi rasilimali yake. Mwekezaji atatazama pia uwezekano wa kupata hasara kwenye njia mbadala ya uwekezaji na kuzilinganisha kabla ya kuamua awekeze wapi.

8. Uundaji wa uwekezaji mseto

Hatari za uwekezaji na faida zake hutofautiana sana kutoka uwekezaji mmoja hadi mwingine. Hisa zinaweza kutoa faida kubwa na ukuaji wa uwekezaji, lakini pia bei ya hisa hubadilika mara kwa mara na hivyo kumfanya mwekezaji kujikuta kwenye hatari ya kupoteza mtaji wake na pia faida itokanayo na uwekezaji huo. Hatifungani kwa upande mwingine hutoa faida yenye uhakika zaidi kutokana na kuwa na uwezekano mdogo wa hasara kulinganisha na hisa. Faida itokanayo na hatifungani ni ndogo kwa kuwa uwezekano wa hasara kwenye hatifungani ni ndogo kuliko kwenye hisa. Mifuko ya uwekezaji wa pamoja kwa upande mwingine inamwezesha mwekezaji kupata ongezeko la thamani na faida nzuri, lakini faida hii hutegemea thamani na uwezekano wa kupata hasara katika vyombo vya uwekezaji ambapo fedha zilizokusanywa huwekezwa.

Uwekezaji mahiri unamhitaji mwekezaji kuweka mseto wa uwekezaji miongoni mwa vyombo kadhaa vya uwekezaji. Uwekezaji mseto ni ule uliojumuisha vyombo mbalimbali vya uwekezaji kama vile hisa, hatifungani, dhamana za serikali kuu na amana za muda maalum. Uwekezaji mahiri unahitaji kuchagua vyombo vya uwekezaji ambavyo vinasaidia kusambaza au kutawanya uwezekano wa kupata hasara. Uwekezaji huu huhitaji kuwekeza kwenye vyombo vya uwekezaji ambavyo faida yake haichangamani sana. Uwekezaji mahiri unahitaji kuchagua uwekezaji ambao faida zake zinaenda kinyume. ikiwa faida inashuka kwenye chombo kimoja cha uwekezaji, itakuwa inaongezeka kwenye chombo kingine, na hivyo kufidia upungufu huo. Kwa ujumla, uwekezaji mahiri utaongeza faida ya mwekezaji kwa

sababu vitega uchumi vilivyochaguliwa husaidia kuongeza faida kwa mwekezaji. Ili kuweza kutawanya hatari za uwekezaji, mwekezaji anahitaji kuwekeza kwenye chombo zaidi ya kimoja. Uwekezaji wa namna hii ni kutawanya mtaji kwenda sehemu mbalimbali.

Mfano:

Kama ilivyoelezwa hapo juu, mseto wa uwekezaji unahusisha kuwekeza kwenye kampuni zaidi ya moja. Kwa mazingira ya Tanzania, mwekezaji aliyenunua hisa kwenye kampuni za bia, sigara, saruji ya Tanga, saruji ya Twiga, na kwenye hatifungani za benki zilizopo kwenye soko la hisa anakuwa amejenga mseto wa uwekezaji. Kwa sasa kuna jumla ya fursa za kuunda mseto wa uwekezaji kupitia hisa za makampuni 10, hatifungani 10 za serikali kuu na tano za makampuni.

9. Jinsi ya kushiriki kwenye masoko ya mitaji

Katika uwekezaji, suala la kujiwekea malengo ni muhimu. Unahitaji kuamua ni nini malengo yako ya uwekezaji na kiasi cha fedha unachotaka kuwekeza, utayari wako kukubali uwezekano wa hasara na kiwango cha uwezekano huo katika uwekezaji, mategemeo yako kuhusu faida kwenye uwekezaji wako na faida hiyo inalipwa mara ngapi kwa mwaka. Utahitaji kugawa mtaji wako kuwekezwa kwenye masoko ya fedha ya muda mfupi na mrefu kulingana na mahitaji yako. Kuwekeza moja kwa moja kwenye masoko ya mitaji kunahitaji kujenga uwekezaji mseto ili uweze kutawanya uwekezaji wako, ukiwa na lengo la kuongeza faida ya uwekezaji wako na kupunguza uwezekano wa kupata hasara.

Kwa upande mwingine, unaweza kuchagua kuwekeza kupitia vyombo vya uwekezaji wa pamoja ambavyo kwa kawaida huwa vimeshatawanya uwekezaji wao kutokana na kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali. Vyombo hivi husaidia wale wasio na utaalam, mtaji wa kutosha kushiriki moja kwa moja kwenye masoko ya mitaji.

Kubainisha hatari ya uwekezaji uliyo tayari kuibeba ni hatua muhimu katika kuamua aina ya mseto wa uwekezaji utakaokuwa nao kwani karibu kila uwekezaji unaambatana na uwezekano wa kupata hasara wa aina fulani. Kwa kuzingatia malengo ya mwekezaji, mikakati, muda wa uwekezaji, utayariwake kukubali uwezekano wa hasara na mategemeo ya faida, mwekezaji anaweza kuchukua mojawapo ya mikakati ifuatayo:

Uwekezaji wa muda mfupi – uwekezaji huu ni wa muda mfupi, chini ya mwaka mmoja. Uwekezaji huu hutegemea mapato ya mwekezaji, umuhimu wa kutunza thamani ya mtaji na urahisi wa kubadilisha uwekezaji ili kupata fedha taslim. Uwekezaji wa muda mfupi kwa mfano, utatenga 50% kwenye bidhaa za uwekezaji katika masoko ya fedha (money markets); 40% kwenye hatifungani na 10% kwenye hisa.

Uwekezaji wa muda wa kati - huu ni uwekezaji wenye kudumu kati ya mwaka mmoja hadi mitatu, ukitegemea kugawanya uwekezaji sawasawa miongoni mwa

vyombo mbalimbali vya uwekezaji. Uwekezaji huu utagawa 40% ya mtaji kwenye hisa; 30% kwenye hatifungani na 30% kwenye dhamana za muda mfupi.

Uwekezaji wa muda mrefu - huu ni uwekezaji wa kuanzia miaka mitatu na kuendelea, ukilenga zaidi ukuaji wa mtaji na faida. Uwekezaji wa muda mrefu unaweza kuwekeza 70% kwenye hisa; 20% kwenye hatifungani na 10% kwenye dhamna za muda mfupi.

Zingatia: Hii ni mifano tu.

10. Ushiriki kwenye masoko ya awali

Masoko ya mitaji yamegawanyika kwenye sehemu kuu mbili, masoko ya awali na masoko ya pili.

10.1. Soko la awali

Hutumika wakati ambapo kampuni inahitaji mtaji na inatoa dhamana zake kwa mara ya kwanza ili kupata mtaji unaotakiwa. Watoaji wa dhamana hizi huomba kibali kwa Mamlaka ili waweze kuuza hisa na hatifungani kukusanya fedha kwa ajili ya kupanua mtaji wao. Watoaji wanatakiwa kuandaa waraka wa matarajio (prospectus) ambao hutoa maelezo yote kuhusu mtoaji ili kumfanya mwekezaji amfahamu mtoaji kabla ya kuwekeza kwenye kampuni husika. Kwa kawaida, soko la awali hudumu kwa muda wa mwezi mmoja, hisa na hatifungani huuzwa kupitia kwa mawakala wa soko la hisa, mabenki, pamoja na wakala walioteuliwa kuuza hisa/hatifungani husika.

10.2. Ushiriki kwenye soko la pili

Soko la pili linahusisha hisa na hatifungani ambazo zimeshatolewa kwenye soko la awali. Soko hili huhusika na hisa na hatifungani ambazo ziko mikononi mwa wawekezaji na wanahitaji fedha na hivyo kuhitaji kuziuza ili wapate fedha zao. Wawekezaji hao huuza hisa au hatifungani kwa bei ya soko ambayo inaweza kuwa tofauti na bei ya soko la awali. Washiriki kwenye soko hili watahitaji kulipa bei ya soko. Kwa mfano hisa za Swissport ziliuzwa kwenye soko la awali mwaka 2003 kwa TZS 225 kila moja. Bei ya hisa moja kwenye soko la pili mwezi Juni 2020 ilikuwa TZS 1,300. Mwekezaji anayetaka kuwekeza Swissport atawajibika kulipa TZS 1,300, ambayo ndio bei ya soko na sio TZS 225. Pamoja na bei hiyo, mwekezaji atatakiwa pia kulipia gharama za uwekezaji ambazo ni 2% ya thamani ya uwekezaji wake.

Ni muhimu kusisitiza kuwa mauzo na manunuzi ya hisa au hatifungani kwenye soko la hisa hufanywa na mawakala wa soko tuu. Wahusika wengine kwenye soko la awali hawahusiki kwenye soko la pili.

10.3. Taratibu za kushiriki kwenye masoko ya awali ya mitaji

Ili kushiriki kwenye masoko ya mitaji mwekezaji anahitaji kufanya yafuatayo:

10.3.1. Wasiliana na wakala wa soko la hisa au benki teule zenye kuuza hisa ili kupata waraka wa matarajio

10.3.2. Soma waraka huo uweze kufahamu kuhusu kampuni inayouza dhamana zake

10.3.3. Ukishaamua kuwekeza, jaza fomu za maombi iliyo kwenye waraka wa matarajio. Hakikisha umeweka maelezo yako yote

10.3.4. Wasilisha maombi na fedha yako kwa wakala wa soko la hisa au benki teule

10.3.5. Wakala wa soko la hisa au benki teule zitawasilisha maombi yako kwa benki inayoratibu makusanyo.

10.3.6. Baada ya kipindi cha mauzo, walioomba kuwekeza watapewa hisa kulingana na maombi yalivyopokelewa.

10.3.7. Vyeti vya umiliki vitatumwa kwa wawekezaji kupitia anuani zilizopo kwenye fomu ya maombi.

10.3.8. Iwapo hukupata hisa kama ulivyoomba, sehemu ya fedha yako itarudishwa. Hali hii hujitokeza pale ambapo maombi ya ununuzi yamezidi thamani ya hisa zilizotolewa kuuzwa kwa umma.

Unaposhiriki kwenye masoko ya mitaji unahitaji kusoma na kuelewa waraka wa matarajio unaobainisha miongoni mwa mambo mengine kama vile mali za kudumu, miundombinu, masoko, ushindani na mazingira. Hivi ni vigezo muhimu vinavyoweza kuongeza uwezekano wa kupata hasara vinavyomkabili mtoaji dhamana na ni lazima mwekezaji aielewe vyema kabla ya kuwekeza katika dhamana. Ni masuala ambayo yanamgusa mtoaji. Kwa mfano katika waraka wa matarajio wa Kampuni ya Cement ya Tanzania (Twiga cement), waliambatanisha maelezo yafuatayo muhimu ambayo ni muhimu wawekezaji, katika toleo la awali, wakayaelewa:

Umiliki wa ardhi – huu ni uwezekano wa kupata hasara unaoweza kukabili kampuni iwapo italazimika kugharamia uhamishaji wa watu watakaojenga kiholela katika ardhi yake kama mahakama itatoa hukumu dhidi ya kampuni husika.

Miundombinu – hii ni gharama ya kufanya biashara Tanzania inayoathiriwa na miundombinu duni hususani barabara za mikoani, treni za mizigo na huduma zingine muhimu.

Masoko na ushindani – Huu ni uwezekano wa hasara unaoambatana na kuunganisha masoko ya nchi jirani pamoja na ushindani wa ndani unaoweza kupunguza nafasi nzuri ya kampuni katika soko.

Uchafuzi wa mazingira – Huu ni uwezekano wa hatua kali zaidi kuchukuliwa ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira. Hii ni pamoja na kubadilika kwa viwango vya kitaifa na kimataifa na hivyo kupelekea kampuni kupata gharama kubwa zaidi na kupunguza ufanisi wake. Uwezekano wa kupata hasara zilizotajwa hapo juu huweza kuathiri mapato na faida ya kampuni. Yameandikwa katika waraka wa matarajio ili kuwatahadharisha wawekezaji watarajiwa wayazingatie kwani

matokeo yake ni kupata mapato ambayo ni kinyume na matarajio ya wawekezaji.

Iwapo mwekezaji ana wasiwasi - awasiliane na wataalamu ambao ni mawakala wa soko la hisa, benki, wahasibu na washauri wa uwekezaji ambao watamsaidia kuelewa na kujibu maswali au dukuduku yoyote aliyokuwa nayo.

11. Kushiriki katika masoko ya mitaji ya pili

Taratibu za kushiriki katika masoko ya mitaji ya pili ni kama zifuatazo:

11.1. Ununuzi

Mwekezaji anayetaka kununua hisa atafuata taratibu zifuatazo:

11.1.1. Wasiliana na wakala wa soko la hisa wa soko la hisa na kumweleza kusudio lako la kununua hisa

11.1.2. Jaza fomu maalum za kununua hisa na kulipia hisa unazotaka kununua

11.1.3. Wakala wa soko la hisa ataweka fedha kwenye akaunti maalum ya benki kwa ajili ya kununua na kuuza hisa za wateja

11.1.4. Wakala wa soko la hisa ataweka oda yako ya kununua hisa kwenye mfumo wa kompyuta wa soko la hisa akitumia namba maalum ya mteja.

11.1.5. Iwapo bei unayotaka kununulia hisa itafanana na bei ya mwekezaji mwingine anayetaka kuuza, basi atakuwa amekununulia hisa hizo. Mwekezaji atapokea cheti cha kuthibitisha kuwa ni mwekezaji kwenye kampuni hiyo.

11.2. Uuzaji

Mwekezaji anayetaka kuuza hisa atafuata taratibu zifuatazo:

11.2.1. Wasiliana na wakala wa soko la hisa na kumweleza kusudio lako la kuuza hisa

11.2.2. Kabidhi hati yako ya umiliki wa hisa kwa wakala wa soko la hisa

11.2.3. Wakala wa soko la hisa atahakiki umiliki wa hisa hizo kabla ya kuuza. Kama hisa haziko kwenye hifadhi ya hisa, wakala wa soko la hisa ataziweka kwenye hifadhi kabla ya kuuza

11.2.4. Wakala wa soko la hisa ataweka oda yako ya kuuza hisa kwenye mfumo wa kompyuta wa soko la hisa akitumia namba maalum ya mteja. Iwapo bei unayotaka kuuzia hisa itafanana na bei ya mwekezaji mwingine anayetaka kununua, basi atakuwa amekuuzia hisa hizo na mwekezaji atalipwa.

Kuna gharama za kushiriki kwenye soko la pili la hisa. Ushuru unaotozwa ni 2% kwa hisa zinazouzwa kwenye soko la hisa la DSM. Vilevile kuna gharama ya kushiriki kwenye soko la pili la vipande vya Mfuko wa Umoja ambavyo vinauzwa

kupitia benki ya CRDB na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT). Wanunuzi na wauzaji kwenye masoko ya pili hulipa ushuru huu. Kwa upande wa vipande, mwekezaji anatakiwa kulipa 1%. Vipande vya Umoja havijaorodheshwa kwenye soko la hisa la DSM kwa sasa. Mauzo na manunuzi kwa upande wa makampuni ambayo hayajaorodheshwa yana taratibu tofauti za mauzo ya hisa zao.

CAPITAL MARKETS AND SECURITIES AUTHORITY

MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA

Afisa Mtendaji Mkuu
Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana
Ghorofa ya 6, Jengo la PSSSF Tower,
Makutano ya Mtaa wa Ohio na Garden,
S.L.P. 75713 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2114959 / 61
Faksi: +255 22 2113846
Barua pepe: info@cmsa.go.tz

Tovuti: www.cmsa.go.tz